


Field Museum   Soldier Field   McCormick Place   Hyde Park   Museum of Science & Industry



### KUTAZAMA KUSINI

Tazama kusini na ufurahie mwonekano wa baadhi ya vivutio vinavyopendwa vya Chicago – kutoka kwa mandhari ya kihistoria ya Soldier Field hadi Field Museum na Museum of Science and Industry. Katika siku isiyo na mawingu, unaweza hata kuona mvuko wa moshi pembezoni mwa Ziwa Michigan ambao unaashiria jiji la viwandani la Gary lililo katika eneo jirani la Indiana.

AON Center   Navy Pier   Millennium Park   Grant Park   Buckingham Fountain   Adler Planetarium   Shedd Aquarium   Northerly Island



### KUTAZAMA MASHARIKI

Tazama mashariki na uburudishe macho yako kwa mandhari ya kushangaza ya mojawapo ya Maziwa makubwa zaidi yenye maji safi, Ziwa Michigan. Arthi inayolizunguka ziwa hilo imesheheni bustani za kupendeza na vivutio vya kitamaduni ikiwemo Millennium Park, Shedd Aquarium, Grant Park, Northerly Island, na Adler Planetarium. Kuelekea mashariki, ng'ambo ya maji, unaweza kuona ufuo wa Michigan.

Wrigley Field   Lincoln Park Zoo   Merchandise Mart   Former John Hancock Center   Water Tower Place




### KUTAZAMA KASKAZINI

Upande wa kaskazini utaona majumba mengi marefu yaliyo na muundo wa kipekee yanayochangia katika umarufu wa mwonekano wa anga la Chicago. Pia utaona Mto Chicago, Lincoln Park Zoo na ukumbi maarufu duniani wa Wrigley Field. Tazama kwenye upeo wa macho na utaanza kuona jinsi ukuaji wa jiji hili umeunganisha mpaka ili kuwiana na majiji ya kusini mwa Wisconsin.



# THE LEDGE

Tufuate  
@SkydeckChicago



THESKYDECK.COM

# SKYDECK



### Asili:

Gundua vyanzo vya Chicago, kumbana na Great Chicago Fire, vumbua jinsi Chicago School of Architecture ilijenga upya jiji, na utembe kwenye Handaki Letu la Reversing the River ili kujifunza kuhusu jiji hili wakati wa miaka ya kuundwa kwake.

### Usanifu wa Mijengo:

Shuhudia usanifu wa mijengo tajika wa Chicago kupitia mkusanyiko wa picha, maonyesho, uhaishaji picha, unaopeperushwa kwenye picha za skirini pana unapoelekea kwenye Mto Chicago! Jifunze kuhusu jumba marufu duniani la Willis Tower – wakati uliopita na uliopo - na uchukue picha za ujuzi wa hali ya juu ukiwa umetulia kando ya pembe za Willis Tower.

### Uwanja wa Michezo wa Jijini:

Zama katika uwasilisho wa nguvu, wa dakika tatu unaofanya Chicago kuwa ya kipekee – sherehe zetu, maeneo muhimu na vivutio vya kitamaduni, hafu za spoti na mengine mengi yatawacha alama ya kudumu!

### Mandhari ya Mitaa:

Ungana na baadhi ya ishara zetu za kimaeneo ikiwemo sahihi yetu ya picha ya "Chicago", ukumbi tajika wa Wrigley Field, Cloud Gate (The Bean), na sanaa ya asili kwenye mitaa.

### Treni ya "L" ya Chicago:

Panda mfano kamili wa treni kamilifu ya "L" ya CTA, keti kwa kiti au ushikilie mtaimbo wa kujishikilia ili kuihisi treni na kufurahia video ya safari wa dakika tatu kupitia maeneo matatu jirani ya Chicago!

### Mionjo ya Chicago:

Pata mwonjo wa macho kwa mapishi marufu ya Chicago na uwe na uhakika wa kujipiga picha ukiwa na pizza yetu kubwa kupindukia na mkate wa hot dog wenye urefu wa futi tisa wa muundo wa Chicago!

### Tabia:

Vumbua ushawishi endelevu wa Chicago kimuziki, spoti, ucheshi, na siasa, hisi msimko kwenye jukwa la pili la jiji, na uchukue picha na watu maarufu kama Michael Jordan, Oprah Winfrey na Barack na Michelle Obama.

### Milango Mahiri:

Milango mahiri ya kisasa inayotambua mguso kiotomatiki inapatikana kwa muda wote wa hali hii kabla ya maonyesho yetu zaidi ya mambo ya kupendeza hisia.

